# SHERIA YA KUWEKA MASHARTI YA UTOAJI LESENI, KUDHIBITI NA KUSIMAMIA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA KWA AJILI YA KUDUMISHA UTULIVU, USALAMA NA UBORA WA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU

**VIFUNGU** **MAELEZO**

**SEHEMU YA KWANZA**
**MASHARTI YA AWALI**

1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Matumizi.
3. Ufafanuzi.

**SEHEMU YA PILI**
**WATOA HUDUMA WA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA**

4. Huduma ya huduma ndogo za fedha.
5. Madaraja ya watoa huduma wa huduma ndogo za fedha.
6. Zuio la kutoa huduma ndogo za fedha.
7. Vikwazo kwa shughuli ndogo za fedha.
8. Mabadiliko ya watoa huduma wa huduma ndogo za fedha.
9 Kiwango cha chini cha mtaji, mali za ukwasi na masharti ya ufilisi.
10. Muundo wa viwango vya riba, faida au tozo.
11. Sehemu ya kutoa huduma.
12. Uendeshaji wa mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha.
13. Uwajibikaji wa watoa huduma wa huduma ndogo za fedha.

## SEHEMU YA TATU
## MASHARTI YA KIUTAWALA


14. Majukumu ya Waziri.

15. Kazi za Benki.

16. Uwezo wa Benki.

17. Kukasimu uwezo na kazi za Benki.


## SEHEMU YA NNE
## UTOAJI WA LESENI KWA WATOA HUDUMA WA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA KWA DARAJA LA PILI NA TATU


18. Maombi ya Leseni.

19. Utoaji wa leseni.

20. Kukataliwa kupewa leseni.

21 Uhalali wa leseni.

22. Kuomba upya.

23. Kufutwa kwa leseni.

24. Athari ya kufutwa leseni.

25. Kufungwa kwa huduma.


## SEHEMU YA TANO
## USAJILI WA WATOA HUDUMA WA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA KWA DARAJA LA NNE


26, Maombi ya usajili kwa Daraja la Nne.

27. Cheti cha usajili.

28. Kukataliwa usajili kwa Daraja la Nne.

29. Athari za usajili.

30. Muda wa usajili.

31. Kufutwa kwa cheti cha usajili.

## SEHEMU YA SITA
## USIMAMIZI NA UANGALIZI WA WATOA HUDUMA WA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA


32. Usimamizi na uchukuaji wa kazi.

33. Ulipaji wa gawio.

34. Vitabu vya hesabu na kumbukumbu nyengine.

35. Mwaka wa Fedha.

36. Uandaaji wa hesabu.

37. Ukaguzi wa hesabu.

38. Mkaguzi wa ndani.

39. Utoaji wa taarifa za fedha.

40. Kutoa taarifa za mikopo.

41. Majukumu ya afisa muhusika wa huduma ndogo za fedha.

42. Uangalizi wa watoa huduma wa huduma ndogo za fedha.

43. Uangalizi maalumu wa mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha.

44. Kufilisiwa kwa mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha.

45. Wajibu wa kumkagua mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha.

46. Uwasilishaji wa taarifa za kipindi.

47. Kufuata Sheria ya Udhibiti wa Utakatishaji Fedha Haramu na Mapato yatokanayo na Uhalifu, Nam. 10 ya 2009.

48. Upatikanaji wa taarifa.

49. Kutunza siri.


## SEHEMU YA SABA
## ULINZI WA MTUMIAJI WA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA


50. Misingi ya kumlinda mtumiaji.

51. Masharti ya mikataba ya mkopo.

52. Ukusanyaji na urejeshaji wa madeni.

## SEHEMU YA NANE
## MASHARTI MENGINEYO


53. Adhabu ya jumla.

54. Dhima kwa matendo yanayotendwa na mjumuiko wa watu.

55. Kumaliza makosa.

56. Huduma ndogo za fedha kwa misingi ya kiislamu.

57. Jukwaa la Mashauriano.

58. Rufaa.

59. Taarifa kwa umma.

60. Ushirikishwaji wa wazawa.

61. Kanuni.

62. Kufuta na kubakiza.

**SHERIA NAM. 9 YA 2023**

**NIMESAINI**

**{DKT. HUSSEIN ALI MWINYI}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

.....1 Februari....., **2024**

# SHERIA YA KUWEKA MASHARTI YA UTOAJI LESENI, KUDHIBITI NA KUSIMAMIA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA KWA AJILI YA KUDUMISHA UTULIVU, USALAMA NA UBORA WA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Zanzibar, 2023 na itaanza kutumika mara baada ya kutiwa saini na Rais na kwa tarehe itakayotangazwa na Waziri katika Gazeti.

Matumizi.

**2.** Sheria hii itatumika katika masuala yote yanayohusiana na huduma ndogo za fedha Zanzibar ikijumuisha huduma ndogo za fedha zinazoendeshwa kwa Misingi ya Kiislamu.

Ufafanuzi.

**3.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo:

"Benki" ina maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Nam. 4 ya 2006;

"benki" ina maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha, Nam. 5 ya 2006;

"Chombo cha Ubadilishanaji wa Taarifa za Mikopo" maana yake ni taasisi mahsusi inayokusanya na kuuza taarifa za mwenendo wa mikopo ya watu binafsi na taasisi;

"huduma ndogo za fedha" maana yake ni kuongeza mikopo midogo, kupokea akiba na kutoa huduma nyengine za fedha kama ilivyoainishwa katika Sheria hii;

"kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii" maana yake ni kikundi kilichoundwa na kusimamiwa kwa pamoja na wanachama ambacho kimesajiliwa chini ya Sheria hii kufanya huduma ndogo za fedha ikijumuisha ukusanyaji wa akiba kutoka kwa wanachama wake na utoaji mikopo kwa wanachama wake lakini haijumuishi:

(a) vikundi vya kijamii vya kusaidiana vilivyoundwa kwa madhumuni ya usalama na ustawi wa jamii na kiuchumi wa wanachama wake ambavyo havipokei akiba na vinatoa mikopo kwa wanachama wake kwa madhumuni ya kutoa huduma ndogo za fedha;

(b) vikundi vya watu wenye maslahi maalumu, vilabu na vyama vinavyokusanya michango ya fedha kutoka kwa wanachama au vinavyopokea michango ya sadaka, vilivyoundwa na kusajiliwa chini ya Sheria ya Vyama vya Ushirika Zanzibar, Nam. 15 ya 2018; na

(c) vikundi vilivyoundwa vya muda mfupi kwa madhumuni ya kupokea michango au upokeaji wa fedha kwa shughuli za kidini au matukio ya kijamii ikijumuisha ndoa au mambo mengine ya kimila yanayohusu familia kwa mtu mmoja mmoja au makundi;

"Mamlaka Iliyokasimiwa" maana yake ni taasisi ya umma iliyokasimiwa mamlaka na Benki kutekeleza kazi na uwezo wa Benki chini ya Sheria hii;

"Mamlaka ya Serikali za Mitaa" ina maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa Zanzibar, Nam. 7 ya 2014;

"Mkopeshaji fedha binafsi" maana yake ni mtu aliyepewa leseni ya kutoa huduma ndogo za fedha ya kukopesha fedha kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii;

"Mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha" maana yake ni taasisi au mtu aliyesajiliwa au aliyepewa leseni ya kufanya huduma ndogo za fedha chini ya Sheria hii;

“Mtoa huduma wa kigeni wa huduma ndogo za fedha” maana yake ni mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha aliyesajiliwa Zanzibar na ambaye wamiliki au wanahisa wake wengi ni wageni;

“mtumiaji” maana yake ni mteja au mwanachama wa mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha ambaye anapata au anakusudia kupata huduma za mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha;

“SACCOS" ina maana kama iliyotafsiriwa katika Sheria ya Vyama vya Ushirika Zanzibar, Nam. 15 ya 2018;

“Taasisi ya fedha” ina maana kama ilivyotafsiriwa na Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha, Nam. 5 ya 2006;

“uhalifu wa kifedha” maana yake ni jambo lolote kati ya yafuatayo:

(a) kosa ambalo linalohusisha wizi, ulaghai, kughushi au kutoa nyaraka ya kughushi, uwongo au kosa liliopo chini ya Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar, Nam. 5 ya 2023 au Sheria ya Udhibiti wa Utakatishaji wa Fedha Haramu na Mapato Yatokanayo na Uhalifu, Nam. 10 ya 2009;

(b) kufadhili, kuwezesha au kuhusika katika kufadhili au kuwezesha kosa linalohusiana na taasisi ya fedha;

(c) kujihusisha na mapato yatokanayo na kosa, yawe yanahusiana au hayahusiani na taasisi ya fedha; na

(d) kosa lolote la uhalifu wa kifedha lililotajwa na sheria yoyote ya Zanzibar;

“Waziri” maana yake ni Waziri anayehusika na fedha.

## SEHEMU YA PILI
## WATOA HUDUMA WA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA

Huduma ya huduma ndogo za fedha.

**4.-**(1) Watoa huduma wa huduma ndogo za fedha waliosajiliwa kwa mujibu wa sheria zao husika watatambuliwa chini ya Sheria hii.

(2) Watoa huduma wa huduma ndogo za fedha chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, watatoa huduma ndogo za fedha kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii.

(3) Bila ya kuathiri masharti ya jumla ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, huduma ya huduma ndogo za fedha zitakazofanywa chini ya Sheria hii, zitajumuisha:

(a) kupokea akiba na kutoa mikopo au huduma nyengine za kukopesha kwa wafanyabiashara wadogo wadogo au wadogo na kaya za kipato cha chini au watu binafsi;

(b) kupokea fedha kwa njia ya amana au riba inayotokana na amana au kukopa na ambayo inakopeshwa kwa wanachama au wateja;

(c) kutoa mikopo midogo, akiba ndogo, bima ndogo, mikopo midogo ya kukodisha, pensheni ndogo na mikopo midogo ya nyumba;

(d) huduma za kuhaulisha na malipo ya fedha ikijumuisha huduma ndogo za fedha kwa njia ya mtandao;

(e) kufanya huduma ya huduma ndogo za fedha za bidhaa ikijumuisha kutoa mikopo ya bidhaa;

(f) kutoa elimu ya fedha; na

(g) huduma nyengine yoyote inayohusiana na hizo kama itakavyoainishwa katika kanuni.

(4) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (3)(c) cha kifungu hiki, masharti kuhusiana na viwango vya mikopo midogo, akiba ndogo, bima ndogo, mikopo midogo ya kukodisha, pensheni ndogo na mikopo midogo ya nyumba vitaainishwa katika kanuni.

Madaraja ya watoa huduma wa huduma ndogo za fedha.

5.-(1) Kwa madhumuni ya Sheria hii, kutakuwa na Madaraja manne ya watoa huduma wa huduma ndogo za fedha kama ifuatavyo:

(a) Daraja la Kwanza litajumuisha taasisi za huduma ndogo za fedha zinazopokea amana;

(b) Daraja la Pili litajumuisha watoa huduma wa huduma ndogo za fedha wasiopokea amana kama vile wakopeshaji;

(c) Daraja la Tatu litajumuisha Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo; na

(d) Daraja la Nne litajumuisha vikundi vya huduma ndogo za fedha vya kijamii.

(2) Watoa huduma wa huduma ndogo za fedha chini ya kifungu kidogo cha (1) (a) cha kifungu hiki, watasimamiwa kwa mujibu wa Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha, Nam. 5 ya 2006.

Zuio la kutoa huduma ndogo za fedha.

**6.**-(1) Mtu hatofanya huduma ndogo za fedha isipokuwa mtu huyo amepewa leseni na amesajiliwa kama mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha na anatoa huduma hiyo kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

(2) Mtu yeyote ambaye anakiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, ametenda kosa na akitiwa hatiani:

(a) kwa upande wa Daraja la Pili, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Ishirini na Tano za Kitanzania na isiyozidi Shilingi Milioni Mia Moja za Kitanzania au kifungo kisichopungua miaka mitatu na kisichozidi miaka mitano au vyote viwili faini na kifungo; na

(b) kwa upande wa Daraja la Tatu, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Kumi na Tano za Kitanzania na isiyozidi Shilingi Milioni Hamsini za Kitanzania au kifungo kisichopungua miaka miwili na kisichozidi miaka mitano au vyote viwili faini na kifungo.

(3) Bila ya kuathiri masharti chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, endapo mtu atatoa mkopo kwa mtu mwengine wakati wa kutoa huduma ndogo za fedha ambayo inafanywa kinyume na kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki:

(a) riba au faida haitolipwa kwa mkopo au malipo ya awali; na

(b) jumla ya mtaji wa mkopo au malipo ya awali hayatarejeshwa kutoka kwa mkopaji isipokuwa Mahakama yenye uwezo, kwa ombi la mkopeshaji, imeridhia kuwa mkopeshaji ameshindwa kufuata masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki.

(4) Masharti ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, yatatumika endapo kulifunguliwa au hakukufunguliwa mashtaka kwa kosa lililotajwa katika kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki.

Katazo kwa shughuli ndogo za fedha.

**7.**-(1) Mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha hatojihusisha katika shughuli yoyote iliyokatazwa chini ya Sheria hii.

(2) Waziri, kupitia kanuni, ataainisha shughuli zinazoruhusiwa na zisizoruhusiwa za watoa huduma wa huduma ndogo za fedha.

(3) Endapo mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha atashindwa kufuata masharti ya kifungu hiki, Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa itachukua hatua kwa mujibu wa sheria kuhakikisha masharti yanafuatwa.

Mabadiliko ya watoa huduma wa huduma ndogo za fedha.

**8.**-(1) Mtoa huduma yeyote wa huduma ndogo za fedha anaweza, baada ya kufikia vigezo vinavyohitajika, kuomba kubadilishwa kutoka Daraja lake husika kwenda Daraja jengine.

(2) Endapo mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha anabadilika kwenda Daraja jengine, mtoa huduma huyo wa huduma ndogo za fedha atasimamiwa kwa mujibu wa sheria zinazosimamia Daraja husika na Sheria hii.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, vigezo vya kubadilika Daraja kwa mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha vitajumuisha:

(a) kiwango cha chini cha mtaji kinachohitajika;

(b) idadi ya wanachama na wateja;

(c) aina ya huduma ya huduma ndogo ya fedha; na

(d) vigezo vyengine vyovyote vinavyohusika vilivyoainishwa katika kanuni.

(4) Bila ya kujali masharti ya kifungu hiki, Benki inaweza, kabla ya kuelekeza mabadiliko ya watoa huduma wa huduma ndogo za fedha, kufanya tathmini inayohusiana na uendelevu wa watoa huduma wa huduma ndogo za fedha baada ya mabadiliko.

(5) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (4) cha kifungu hiki, endapo Benki imejiridhisha kwamba mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha amekidhi vigezo vya mabadiliko, inaweza kuelekeza mabadiliko ya mtoa huduma huyo wa huduma ndogo za fedha kwa kuzingatia vigezo na masharti.

(6) Endapo mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha, bila sababu za msingi, ameshindwa kufuata maelekezo yaliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (5) cha kifungu hiki, Benki itachukua hatua stahiki kama itakavyoona inafaa ili kuhakikisha maelekezo yanafuatwa.

Kiwango cha chini cha mtaji, mali za ukwasi na masharti ya ufilisi.

**9.** Mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha ambaye anatoa huduma ya huduma ndogo za fedha chini ya Sheria hii, atafuata mahitaji ya kiwango cha chini cha mtaji, kiwango cha chini cha mali za ukwasi na uwiano wa ufilisi kama ilivyoainishwa katika kanuni.

Muundo wa viwango vya riba, faida au tozo.

**10.** Mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha ataweka muundo wa viwango vya riba, faida au tozo ambao unaruhusu kurejesha gharama zake za uendeshaji ikijumuisha gharama ya mtaji na hasara ya mikopo kama itakavyoamuliwa na Benki.

Sehemu ya kutoa huduma.

**11.**-(1) Kila mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha atakuwa na sehemu ya kutoa huduma yenye anuani sahihi kwa ajili ya kutoa huduma.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha hatofungua au kufunga sehemu ya huduma bila ya idhini ya awali ya Benki au Mamlaka iIliyokasimiwa.

(3) Mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha ambaye anakiuka masharti ya kifungu hiki, ametenda kosa na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Moja za Kitanzania na isiyozidi Shilingi Milioni Tano za Kitanzania.

Uendeshaji wa watoa huduma wa huduma ndogo za fedha.

**12.**-(1) Uendeshaji wa watoa huduma wa huduma ndogo za fedha utakuwa kama ilivyoainishwa katika sheria zao anzilishi, katiba au sheria ndogo husika.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa inaweza, iwapo ikiwa imejiridhisha kuwa taratibu za uendeshaji za mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha haziendani na huduma ya huduma ndogo za fedha, itatoa maelekezo ya jumla au maalumu kwa mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha kuhusu uendeshaji wake na maelekezo hayo yatapaswa kufuatwa.

Uwajibikaji wa mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha.

**13.** Mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha, kwa madhumuni ya kutoa huduma ndogo za fedha, atawajibika kwa Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa.

## SEHEMU YA TATU
## MASHARTI YA KIUTAWALA

Majukumu ya Waziri.

**14.**-(1) Waziri ataandaa na kusimamia utekelezaji wa sera ya huduma ndogo za fedha kwa madhumuni ya kuhakikisha mazingira mazuri ya huduma ya huduma ndogo za fedha.

(2) Kwa madhumuni ya masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Waziri:

(a) ataimarisha mazingira wezeshi ya kusaidia huduma ya huduma ndogo za fedha;

(b) atahakikisha ukuaji, uwazi, uwajibikaji na uendelevu wa huduma ya huduma ndogo za fedha;

(c) atatoa maelekezo kwa Benki katika utekelezaji wa sera yanayohusiana na utoaji wa huduma ndogo za fedha; na

(d) atatekeleza jukumu jengine lolote kwa utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

(3) Katika kutekeleza majukumu yake chini ya kifungu hiki, Waziri anaweza, baada ya kushauriana na Waziri husika, kuagiza au kutaka taarifa au nyaraka zinazohusu utoaji wa huduma ndogo za fedha kutoka Wizarani, taasisi au ofisi na Wizara, taasisi au ofisi hiyo inapaswa kutekeleza.

(4) Waziri anaweza, kwa kushauriana na Waziri anayehusika na vyama vya ushirika au Waziri anayehusika na Mamlaka za Serikali za Mitaa kama itakavyokuwa, kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa wajibu wake chini ya Sheria hii.

Kazi za Benki.

15.-(1) Benki itakuwa na jukumu la kusimamia na kufuatilia watoa huduma wa huduma ndogo za fedha kwa mujibu wa Sheria hii.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kazi za Benki zitakuwa ni kudhibiti na kusimamia uendeshaji wa utoaji wa huduma ndogo za fedha kwa mujibu wa Sheria hii na sheria nyengine yoyote inayohusika.

(3) Bila ya kuathiri masharti ya jumla ya vifungu vidogo vya (1) na (2) vya kifungu hiki, Benki:

(a) itatoa leseni kwa watoa huduma wa huduma ndogo za fedha waliokidhi vigezo kwa mujibu wa Sheria hii;

(b) itamshauri na kuwasilisha taarifa kwa Waziri juu ya masuala yanayohusiana na huduma ya huduma ndogo za fedha;

(c) itaanzisha na kusimamia kanzidata kwa ajili ya watoa huduma wa huduma ndogo za fedha;

(d) itatoa matoleo na miongozo kwa watoa huduma wa huduma ndogo za fedha;

(e) itakuza viwango vya mwenendo mzuri wa huduma na taratibu za kifedha Zanzibar;

(f) itakagua, itafuatilia na kutathmini utendaji wa huduma ndogo za fedha;

(g) itahakikisha usimamizi bora wa malalamiko yanayohusiana na huduma ya huduma ndogo za fedha;

(h) itatathmini na kutoa idhini kwa ajili ya mabadiliko ya watoa huduma wa huduma ndogo za fedha kutoka Daraja moja kwenda Daraja jengine;

(i) itahakikisha ulinzi kwa watumiaji wa watoa huduma wa huduma ndogo za fedha ikijumuisha kutoa adhabu kwa ukopeshaji mbaya unaokwenda kinyume na utaratibu wa ukopeshaji;

(j) itahakikisha kwamba taarifa za mikopo inayohusiana na utoaji wa huduma ndogo za fedha zinakusanywa, zinasambazwa na zinapatikana kwa urahisi; na

(k) itatekeleza kazi nyengine kama itakavyotakiwa kwa ajili ya udhibiti na usimamizi mzuri wa utoaji wa huduma ndogo za fedha.

Uwezo wa Benki.

**16.** Benki, katika kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria hii, itakuwa na uwezo wa:

(a) kuchunguza au kuhoji uendeshaji wa shughuli za watoa huduma wa huduma ndogo za fedha;

(b) kutaka kupatiwa taarifa zinazohusiana na shughuli za watoa huduma wa huduma ndogo za fedha;

(c) kuelekeza katika usimamizi bora wa watoa huduma wa huduma ndogo za fedha;

(d) kuingia kwa muda unaofaa, katika eneo lolote la mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha au eneo lolote ambalo inaaminika kwa sababu za msingi, kwamba vitabu vya hesabu, kumbukumbu au nyaraka katika muundo wowote zinazohusiana na huduma za mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha zinatunzwa;

(e) kukagua na kuchunguza vitabu vya hesabu, kumbukumbu, marejesho na nyaraka nyengine zozote za watoa huduma wa huduma ndogo za fedha;

(f) kufungua au kuwezesha kufunguliwa kwa chumba maalumu, kasha au chombo chengine cha kuhifadhia fedha ambacho ndani yake kinashukiwa kwa sababu za msingi kwamba, kuna dhamana, vitabu vya hesabu, kumbukumbu au nyaraka zozote za mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha;

(g) kumtaka afisa, muajiriwa au wakala yeyote wa mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha kutoa au kuwasilisha maelezo au nyaraka zinazohusu usimamizi au shughuli za mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha; na

(h) kutekeleza uwezo huo kama itakavyokuwa muhimu kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu yake chini ya Sheria hii.

Kukasimu uwezo na kazi za Benki.

**17.**-(1) Benki inaweza, kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa kazi na uwezo wake wa udhibiti na usimamizi chini ya Sheria hii na kwa kuzingatia masharti na taratibu maalum ambazo Benki itaweka, kwa tangazo litakalochapishwa katika Gazeti kukasimu kazi au uwezo wake wowote unaohusiana na mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha:

(a) katika Daraja la Tatu, kwa Idara ya Maendeleo ya Ushirika iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Vyama vya Ushirika Zanzibar, Nam. 15 ya 2018; na

(b) katika Daraja la Nne, kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kama zilivyoanzishwa chini ya Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa Zanzibar, Nam. 7 ya 2014.

(2) Mamlaka Iliyokasimiwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itatekeleza kazi na uwezo kwa mujibu wa masharti, taratibu na maelekezo mengine yoyote yatakayotolewa na Benki kila baada ya muda.

(3) Uwezo au kazi yoyote iliyokasimiwa chini ya kifungu hiki, itakapotekelezwa au kufanywa na Mamlaka Iliyokasimiwa, itachukuliwa kama imetekelezwa au kufanywa na Benki.

(4) Bila ya kujali masharti chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, isipokuwa kama itaidhinishwa vyenginevyo na Waziri, Benki haitokasimu kazi na uwezo wake kuhusiana na udhibiti na usimamizi wa watoa huduma wa huduma ndogo za fedha katika Daraja la Pili.

## SEHEMU YA NNE
## UTOAJI WA LESENI KWA WATOA HUDUMA WA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA KWA DARAJA LA PILI NA TATU

Maombi ya Leseni.

**18.**-(1) Mtu ambaye anakusudia kutoa huduma ya huduma ndogo za fedha chini ya Daraja la Pili ataomba leseni kwa Benki kwa namna kama ilivyoelezwa katika kanuni.

(2) Mtu ambaye anakusudia kutoa huduma ya huduma ndogo za fedha chini ya Daraja la Tatu ataomba leseni kwa Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa kwa namna kama ilivyoelezwa katika kanuni.

(3) Mtoa huduma wa kigeni wa huduma ndogo za fedha ambaye anataka kutoa huduma ndogo za fedha Zanzibar ataomba leseni kwa Benki kwa namna kama ilivyoelezwa katika kanuni.

(4) Endapo mtoa huduma wa kigeni wa huduma ndogo za fedha anatoa huduma ndogo za fedha Zanzibar, mtoa huduma huyo atafuata sheria zinazotumika.

(5) Baada ya kupokea maombi chini ya Sheria hii, Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa inaweza, ndani ya muda ulioainishwa katika kanuni, kuzingatia kama maombi yamefuata masharti yaliyowekwa.

Utoaji wa leseni.

**19.**-(1) Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa, ndani ya miezi mitatu baada ya kupokea maombi, itazingatia maombi na kama imejiridhisha kwamba muombaji amekidhi vigezo, itatoa leseni kwa muombaji.

(2) Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa itatoa leseni kwa kuzingatia vigezo na masharti kama ilivyoainishwa katika kanuni.

(3) Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa, kabla ya kutoa leseni, itazingatia masuala yote itakayoona ni muhimu kwa maombi ikijumuisha:

(a) iwapo utoaji wa huduma ndogo za fedha utaendeshwa na watu ambao wanafaa na sahihi;

(b) asili ya rasilimali fedha ya muombaji kama ni chanzo cha fedha endelevu cha kumsaidia mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha; na

(c) ufanisi wa mpango wa huduma uliowasilishwa na muombaji kwa ajili ya uendeshaji na maendeleo ya baadae ya huduma ya taasisi ya huduma ndogo za fedha.

*Kukataliwa kupewa leseni.*

**20.**-(1) Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa inaweza kukataa kutoa leseni iwapo:

(a) muombaji ameshindwa kukidhi vigezo na masharti yaliyoainishwa ya leseni; au

(b) muombaji ametoa taarifa za kupotosha au zisizo sahihi zinazohusiana na maombi.

(2) Endapo Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa itakataa kutoa leseni, ndani ya siku kumi za kazi kuanzia tarehe ya uamuzi wake, itamtaarifu muombaji kwa maandishi sababu za kukataa kwake.

*Uhalali wa leseni.*

**21.** Leseni iliyotolewa chini ya Sheria hii itaanza kutumika kutoka tarehe ya kutolewa kwa leseni na itakuwa halali kwa kipindi chote isipokuwa kama itafutwa na Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa.

*Kuomba upya.*

**22.**-(1) Muombaji ambaye maombi yake yamekataliwa anaweza kuomba upya, iwapo mapungufu ya msingi yaliyosababisha kukataliwa kwa maombi ya awali au mapitio yaliyofuata yamerekebishwa.

(2) Maombi mapya chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, hayatatumika kwa mapungufu yaliyoainishwa chini ya kifungu cha 20(1)(b) cha Sheria hii.

*Kufutwa kwa leseni.*

**23.**-(1) Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa inaweza, kwa taarifa ya maandishi, kufuta leseni iliyotolewa chini ya Sheria hii endapo imejiridhisha kwamba, mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha:

(a) hajaanza kutoa huduma ndani ya miezi sita kutoka tarehe ya kutolewa leseni;

(b) ameacha kutoa huduma ndogo za fedha ambayo leseni ilitolewa;

(c) amewasilisha taarifa au nyaraka yoyote ya uongo au ya kupotosha kuhusiana na maombi ya leseni;

(d) amebainika kuwa amefilisika au hawezi kulipa madeni yake;

(e) amefungiwa, amefilisiwa au amefutwa;

(f) amejihusisha na udanganyifu kuhusiana na hali yake ya kifedha, umiliki, usimamizi, uendeshaji au mambo mengine muhimu kwa huduma yake;

(g) bila ya kupata ridhaa ya Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa ameunganishwa na kampuni nyengine au ameuza au vyenginevyo amehamisha mali na madeni yake kwa kampuni nyengine;

(h) anatoa huduma katika namna ambayo anaathiri maslahi ya wenye amana au wateja wake;

(i) ameendelea kukiuka masharti ya Sheria hii;

(j) ameshindwa kufuata masharti yoyote yaliyoainishwa katika leseni yake;

(k) amehaulisha au amempa leseni yake mtu mwengine; au

(l) ameshindwa kuwasilisha au kutoa taarifa ya ukaguzi wa vitabu vya hesabu na nyaraka nyengine zinazohusika chini ya Sheria hii.

(2) Utaratibu wa kufutwa leseni utakuwa kama ulivyoainishwa katika kanuni.

Athari ya kufutwa leseni.

**24.**-(1) Endapo leseni ya mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha itafutwa kwa mujibu wa Sheria hii, Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa itaondoa jina la mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha kutoka kwenye daftari la kumbukumbu na kwa maandishi itamuelekeza mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha huyo:

(a) kusimamisha shughuli zake kuanzia tarehe ya kufutwa kwa leseni;

(b) kusimamia na kushughulikia, ndani ya muda kama utakavyoainishwa, masuala yote yanayohusu mali na madeni ya watumiaji au wanachama; na

(c) kukabidhi leseni iliyofutwa.

(2) Endapo mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha ameshindwa kutekeleza maelekezo yaliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa itakuwa na uwezo wa kuchukua hatua yoyote, kama itakavyoona inafaa, kulinda haki za watumiaji au wanachama.

Kufungwa kwa huduma.

**25.**-(1) Mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha ataomba idhini kutoka kwa Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa kabla ya kufunga huduma yake.

(2) Kwa kuzingatia masharti chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, ombi la kufunga huduma litaambatanishwa na taarifa ya fedha ya huduma kama ilivyoainishwa na Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa.

## SEHEMU YA TANO
## USAJILI WA WATOA HUDUMA WA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA KWA DARAJA LA NNE

Maombi ya usajili kwa Daraja la Nne.

**26.** Ombi la usajili kama mtoa huduma wa huduma ndogo ya fedha kwa Daraja la Nne litaombwa kwa Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa kwa namna kama ilivyoainishwa katika kanuni.

Cheti cha usajili.

**27.**-(1) Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa, ndani ya siku kumi za kazi baada ya kupokea ombi, itatoa cheti cha usajili au kukataa ombi.

(2) Cheti cha usajili kilichotolewa chini ya kifungu kidogo cha (l) cha kifungu hiki, kitajumuisha taarifa kama zilivyoainishwa katika kanuni.

Kukataliwa usajili kwa Daraja la Nne.

**28.** Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa itakataa kumsajili muombaji ikiwa:

(a) muombaji huyo:

(i) ameshindwa kukidhi masharti yaliyowekwa ya usajili au alitoa taarifa za uongo wakati wa usajili; au

(ii) amejihusisha katika shughuli ambazo zimepelekea utoaji wa huduma ndogo za fedha katika sifa mbaya kama ilivyoelezwa na Sheria hii; au

(b) mtu yeyote anayehusika na usimamizi wa taasisi iliyoomba, ametiwa hatiani kwa kosa linalohusiana na wizi, ulaghai, kukosa uaminifu au uhalifu mwengine wowote wa kifedha ikiwa ndani ya Zanzibar au nje

ya Zanzibar katika kipindi cha miaka saba iliyopita chini ya sheria yoyote.

Athari za usajili.

**29.**-(1) Cheti cha usajili kitakuwa ni ushahidi kamili wa mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha kuendesha au kutoa huduma ndogo za fedha kwa mujibu wa katiba yake na masharti ya Sheria hii.

(2) Mtu ambaye anajihusisha na utoaji wa huduma ndogo za fedha chini ya Daraja la Nne bila ya kusajiliwa kwa mujibu wa Sheria hii, ametenda kosa.

Muda wa usajili.

**30.** Usajili wa mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha utaendelea kutumika hadi utakapofutwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

Kufutwa kwa cheti cha usajili.

**31.**-(1) Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa inaweza kufuta cheti cha usajili ikiwa imejiridhisha kuwa:

(a) vigezo au masharti yaliyowekwa katika cheti cha usajili yamekiukwa;

(b) mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha ameacha kutoa huduma; au

(c) mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha anatoa huduma yake kinyume na masharti ya Sheria hii au sheria nyengine husika.

(2) Endapo cheti cha usajili kimefutwa, Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa:

(a) itamtaarifu mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha husika kwa maandishi sababu za kufutwa kwa usajili;

(b) itamuagiza mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha kusitisha shughuli zake; na

(c) itaondoa jina la mtoa huduma huyo wa huduma ndogo za fedha katika daftari la kumbukumbu.

(3) Masharti ya Sheria hii yanayohusiana na taratibu za kufutwa kwa leseni yatatumika sawa na kufuta cheti cha usajili chini ya Sheria hii.

## SEHEMU YA SITA
## USIMAMIZI NA UANGALIZI WA WATOA HUDUMA WA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA

Usimamizi na uchukuaji wa kazi.

**32.**-(1) Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa inaweza kuchukua usimamizi wa kazi ya mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha endapo inaona kwamba, mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha:

(a) hayupo katika hali nzuri ya kifedha;

(b) hafanyi kazi kwa mujibu wa mwenendo unaokubalika wa taratibu za kiutawala na uhasibu;

(c) hazingatii sera zinazofaa za usimamizi wa viashiria hatarishi;

(d) ameshindwa kufuata masharti ya kiwango cha chini cha mtaji yaliyoainishwa chini ya Sheria hii;

(e) anatoa huduma ndogo za fedha katika utaratibu ambao upo kinyume na Sheria hii;

(f) anakataa kukaguliwa na Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa kama inavyotakiwa na Sheria hii;

(g) leseni yake imefutwa; na

(h) kuendelea kwake katika kufanya huduma ndogo za fedha kutaathiri maslahi ya huduma ndogo za fedha.

(2) Muhusika katika mkataba na mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha hataondolewa majukumu yake kwa msingi kwamba mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha yuko chini ya usimamizi wa Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa.

(3) Gharama za usimamizi za mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha wakati wa kipindi cha uchukuaji wa kazi hazitabebwa na Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa.

(4) Utaratibu wa usimamizi na uchukuaji wa kazi za mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha chini ya kifungu hiki, zitakuwa kama ilivyoainishwa katika kanuni. .

Ulipaji wa gawio.

**33.** Mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha atalipa gawio kwa wanahisa wake au atafanya utaratibu mwengine wowote wa ugawaji au malipo ya riba au faida kwa

watumiaji au wanachama wake katika namna kama ilivyoainishwa katika katiba au nyaraka nyengine zinazohusika za mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha.

**Vitabu vya hesabu na kumbukumbu nyengine.**

**34.** Mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha ataweka vitabu sahihi vya hesabu na kumbukumbu nyengine za miamala ya kifedha zinazohusiana na uendeshaji wa huduma zake kwa mujibu wa kanuni au miongozo.

**Mwaka wa Fedha.**

**35.** Mwaka wa fedha wa mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha utakuwa ni kipindi cha miezi kumi na mbili kinachoishia tarehe 31 Disemba kila mwaka kwa mujibu wa kanuni au miongozo.

**Uandaaji wa hesabu.**

**36.**-(1) Isipokuwa kwa watoa huduma chini ya Daraja la Nne, mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha, katika kila mwaka wa fedha, ataandaa hesabu kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya utoaji taarifa za fedha, au katika muundo kama utakavyowekwa na Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa.

(2) Hesabu na kumbukumbu nyengine za fedha za mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha zitawekwa kwa Shilingi ya Kitanzania.

**Ukaguzi wa hesabu.**

**37.**-(1) Hesabu za mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha, isipokuwa chini ya Daraja la Nne, zitakaguliwa angalau mara moja kwa mwaka na mkaguzi kwa namna ilivyoainishwa katika kanuni.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, hesabu na taarifa za fedha za watoa huduma wa huduma ndogo za fedha chini ya Daraja la Nne zitakaguliwa na kusimamiwa kama ilivyoainishwa katika kanuni.

(3) Endapo Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa imejiridhisha kwamba hesabu zilizokaguliwa za mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha hazijakidhi vigezo vya Sheria hii au kanuni husika au zina taarifa ambazo zinaweza kuwa za kupotosha au hazijatangazwa kwa utaratibu ulioainishwa katika fomu maalumu, Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa inaweza kumtaka mtoa huduma:

(a) kurekebisha hesabu zilizokaguliwa ili kutimiza masharti ya Sheria;

(b) kusahihisha taarifa inayopotosha;

(c) kutangaza upya hesabu zilizokaguliwa zilizorekebishwa; na

(d) kuwasilisha kwa Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa nyaraka au taarifa za ziada zinazohusiana na nyaraka au taarifa yoyote.

(4) Endapo mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha, bila ya sababu ya msingi, ameshindwa kufuata masharti ya kifungu hiki, Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa itachukua hatua kwa mujibu wa sheria kuhakikisha masharti yanafuatwa.

Mkaguzi wa ndani.

**38.** Mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha chini ya Daraja la Pili na Daraja la Tatu atakuwa na mtu anayehusika na tathmini ya ufanisi wa mifumo ya udhibiti wa ndani kwa namna ilivyoainishwa katika kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii.

Utoaji wa taarifa za fedha.

**39.**-(1) Mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha atatoa taarifa zake za fedha kwa Benki, Mamlaka Iliyokasimiwa au washirika wake kwa namna kama ilivyoainishwa katika kanuni.

(2) Bila ya kuathiri kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha, kwa kipindi chote cha mwaka na katika eneo lake linaloonekana la huduma, ataweka taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka katika muundo na namna kama itakavyoainishwa na Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa.

(3) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa inaweza kuainisha namna ambavyo mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha katika Daraja la Nne atakavyotoa taarifa zake za fedha.

(4) Endapo mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha, bila ya sababu ya msingi, ameshindwa kufuata masharti ya kifungu hiki, Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa itachukua hatua kwa mujibu wa sheria zinazotumika kama itakavyokuwa inafaa kuhakikisha masharti yanatekelezwa.

Kutoa taarifa za mikopo.

**40.**-(1) Mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha atatoa taarifa za mikopo kwa namna ilivyoainishwa katika kanuni.

(2) Mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha anaweza kupata na kutumia taarifa za mikopo katika Kituo cha Ubadilishaji wa Taarifa za Mikopo kwa namna ilivyoainishwa katika kanuni.

(3) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu hiki, utoaji wa taarifa za mikopo utafanywa kwa mujibu wa Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Nam. 4 ya 2006 na Sheria ya Udhibiti wa Utakatishaji wa Fedha Haramu na Mapato Yatokanayo na Uhalifu, Nam. 10 ya 2009.

(4) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, taarifa ya mikopo itajumuisha taarifa yoyote ikiwemo taarifa binafsi na historia ya mikopo ya mkopaji kama mwenendo wa kulipa wa mtu, madeni ambayo bado hayajalipwa, wajibu wa kodi na maelezo mengine yoyote ya kina ya huduma.

(5) Endapo mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha, bila sababu za msingi, ameshindwa kufuata masharti ya kifungu hiki, Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa itachukua hatua stahiki ili kuhakikisha masharti yanatekelezwa.

Majukumu ya afisa muhusika wa huduma ndogo za fedha.

**41.**-(1) Kila afisa muhusika wa mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha atakuwa na jukumu la uaminifu katika mahusiano, jukumu la kujali na ujuzi kwa huduma ndogo za fedha, hususan:

(a) kufanya kazi kwa nia njema kwa manufaa ya wanachama na wanahisa wake;

(b) kuepuka mgongano wa maslahi;

(c) kuwa na kudumisha taaluma na ujuzi; na

(d) kutekeleza majukumu yake yanayohusiana na taasisi kwa umakini.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, afisa muhusika wa watoa huduma wa huduma ndogo za fedha wote, katika kutekeleza majukumu yao, watafuata miongozo yoyote na kuzingatia vigezo vyovyote vilivyoainishwa kwa mujibu wa sheria na miongozo.

Uangalizi wa watoa huduma wa huduma ndogo za fedha.

**42.** Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa katika uangalizi wa watoa huduma wa huduma ndogo za fedha:

(a) itafuatilia, itachunguza na itatathmini kila baada ya muda, utendaji kazi wa watoa huduma wa huduma ndogo za fedha;

(b) itachambua marejesho ya kisheria;

(c) itachambua hesabu zilizokaguliwa za mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha; na

(d) itakagua na kuchambua kumbukumbu.

Uangalizi maalumu wa mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha.

**43.**-(1) Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa inaweza kumuweka chini ya uangalizi maalumu mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha endapo:

(a) kuna uwezekano kwamba mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha hawezi kukidhi masharti ya wawekaji wake wa amana au kutekeleza wajibu wake wa kulipa katika shughuli za kawaida za kihuduma; au

(b) mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha amepata au ana uwezekano wa kupata hasara ambayo itapunguza mtaji wake wote au kwa kiasi kikubwa.

(2) Taasisi au mtu aliyeteuliwa na Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa atakuwa muangalizi maalumu wa mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha.

Kufilisiwa kwa mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha.

**44.** Bila ya kujali sheria nyengine yoyote, shauri la kufunga au kufilisi mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha halitafunguliwa isipokuwa na:

(a) Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa; au

(b) mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha kwa idhini ya Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa.

Wajibu wa kumkagua mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha

**45.**-(1) Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa itakuwa na wajibu wa kumkagua mtoa huduma yeyote wa huduma ndogo za fedha.

(2) Wakati wa ukaguzi, mtoa huduma wa huduma ndogo ya fedha anayehusika na kila afisa au mfanyakazi atawasilisha na kutoa kwa maandishi, kwa mtu anayefanya ukaguzi, vitabu vyote vya hesabu, kumbukumbu na nyaraka nyengine, barua, maelezo na taarifa nyengine zinazohusiana na huduma kama itakavyohitajika.

(3) Mtu ambaye atashindwa kutoa vitabu, hesabu, kumbukumbu, nyaraka, barua, maelezo au taarifa nyengine yoyote inayohitajika chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, ametenda kosa.

(4) Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa itawasilisha taarifa ya ukaguzi ambayo inajumuisha kuwepo au kutokuwepo:

(a) uvunjwaji au ukiukwaji wowote wa Sheria hii na kanuni zozote zilizotungwa chini yake;

(b) usimamizi mbaya wowote wa mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha;

(c) ukiukwaji wowote wa taratibu za mwenendo wa mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha aliyekaguliwa; na

(d) jambo jengine lolote linalohusiana na mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha ambalo haliendani na utaratibu unaokubalika wa shughuli za huduma.

(5) Endapo Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa, baada ya kuzingatia taarifa ya ukaguzi chini ya kifungu kidogo cha (4) cha kifungu hiki, itaona kwamba shughuli za mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha zinatolewa kwa kuwaathiri watumiaji wake au zinafanywa kinyume na Sheria hii, inaweza, baada ya kumpa mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha nafasi ya kujieleza kuhusiana na taarifa hiyo, kuchukua hatua kwa namna itakavyoona inafaa, ikijumuisha:

(a) kuzuia, kusimamisha au kukataza malipo ya gawio kwa mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha;

(b) kumuelekeza mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha kuchukua hatua ya kinidhamu dhidi ya afisa yeyote aliyehusika na kosa hilo;

(c) kumsimamisha au kumuachisha kazi mkurugenzi, afisa au mfanyakazi aliyefanya kosa;

(d) kumuelekeza mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha kuunda upya uongozi wake;

(e) kumuamuru mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha kuwasilisha kwa Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa ndani ya muda uliowekwa:

(i) mpango wa kurejesha mtaji; au

(ii) mpango wa kutatua kasoro zote kwa namna ambavyo Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa itaridhika;

(f) kumzuia au kumsimamisha mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha asitoe tunzo, nyongeza ya mshahara au maslahi mengine kwa uongozi wa juu au kwa maafisa wa huduma ya huduma ndogo za fedha;

(g) kuweka vikwazo katika ongezeko la mali au madeni ya mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha kwa namna itakavyoona inafaa; na

(h) kumuamuru mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha kufanya au kuchukua hatua nyengine yoyote kama itakavyoona inafaa.

Uwasilishaji wa taarifa za kipindi.

**46.**-(1) Mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha atawasilisha Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa taarifa za kipindi za uendeshaji wake wa huduma zake za huduma ndogo za fedha kwa muda na namna kama ilivyoainishwa katika kanuni.

(2) Endapo mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha, ameshindwa kufuata masharti ya kifungu hiki, Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa itachukua hatua stahiki kama itakavyoona inafaa ili kuhakikisha masharti yanafuatwa.

Kufuata Sheria ya Udhibiti wa Utakatishaji Fedha Haramu na Mapato yatokanayo na Uhalifu, Nam. 10 ya 2009.

**47.**-(1) Mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha atazingatia Sheria ya Udhibiti wa Utakatishaji wa Fedha Haramu na Mapato Yatokanayo na Uhalifu, Nam. 10 ya 2009, kwa kuweka utaratibu wa udhibiti wa ndani kwa madhumuni ya utambuzi na utoaji taarifa ya miamala inayoshukiwa.

(2) Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa itahakikisha kuwa kila mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha anatoa huduma kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki.

Upatikanaji wa taarifa.

**48.**-(1) Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa itakuwa na uwezo wa kupata taarifa zinazohusu shughuli za watoa huduma wa huduma ndogo za fedha wowote na inaweza kuelekeza, kwa maandishi, kwamba taarifa hiyo iwasilishwe ndani ya muda ulioanishwa kwenye maelekezo.

(2) Endapo mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha, bila ya sababu za msingi, ameshindwa kutekeleza masharti ya kifungu hiki, Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa itachukua hatua stahiki kama itakavyoona inafaa kuhakikisha masharti yanatekelezwa.

Kutunza siri.

**49.**-(1) Endapo Benki, Mamlaka Iliyokasimiwa au mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha atapata taarifa inayopatikana chini ya Sheria hii, taarifa hiyo itachukuliwa kuwa ni siri na haitatolewa kwa mtu mwengine yeyote.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa inaweza kutoa taarifa yoyote:

(a) kwa taasisi au mtu aliyeidhinishwa endapo taarifa hiyo inahitajika kwa ajili ya usimamizi au udhibiti na usiri wake utaendelea kulindwa; au

(b) kwa kufuata sheria, amri ya mahakama au kwa ridhaa ya moja kwa moja ya mtumiaji anayehusika.

## SEHEMU YA SABA
## ULINZI WA MTUMIAJI WA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA

Misingi ya kumlinda mtumiaji.

**50.**-(1) Mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha atafuata misingi ya kumlinda mtumiaji kama ilivyoainishwa katika sheria zinazotumika na katika kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, misingi ya kumlinda mtumiaji iliyoainishwa katika kanuni itajumuisha:

(a) vigezo na masharti ya mikopo au huduma zinazohusiana na hizo kuwa za uwazi, usawa, haki na kulinda haki na maslahi ya watumiaji wa huduma ndogo za fedha au wanachama;

(b) ushughulikiaji wa malalamiko na njia za utatuzi wa migogoro;

(c) utoaji kamili wa taarifa husika wa bidhaa na huduma zinazotolewa;

(d) sharti la kuhakiki viwango vya mikataba ya mikopo au makubaliano;

(e) kushiriki kikamilifu katika elimu ya fedha na programu za uelewa kwa watumiaji;

(f) uwazi wa viwango vya riba, faida, tozo au adhabu;

(g) ulinzi wa mali ya mteja dhidi ya udanganyifu na matumizi mabaya; na

(h) msingi mwengine wowote kwa madhumuni ya kuhakikisha usawa katika utoaji wa huduma kwa watumiaji.

(3) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, kigezo au sharti lolote lililoainishwa katika mkataba au nyaraka yoyote husika inayodaiwa kutoa mamlaka kwa mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha, ya kuanzisha au kurekebisha kiwango cha riba au faida kwa upande mmoja au hali nyengine yoyote ya mkopo itakuwa batili.

(4) Endapo mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha, bila ya sababu za msingi, atashindwa kufuata masharti ya kifungu hiki, Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa itachukua hatua hizo kadri itakavyokuwa sahihi ili kuhakikisha masharti yanafuatwa.

(5) Kwa madhumuni ya kifungu hiki "misingi ya kumlinda mtumiaji" inajumuisha misingi iliyokusudiwa kuhakikisha uwazi wa bidhaa na huduma zinazotolewa na watoa huduma wa huduma ndogo za fedha, usawa katika utoaji wa huduma na ulinzi wa maslahi na haki za mtumiaji pamoja na usikilizaji wa haki wa malalamiko na njia za utatuzi wa migogoro, kuepuka kuwa na madeni mengi na kuhakikisha kwamba mikopo itatolewa kwa wakopaji.

Masharti ya mikataba ya mkopo.

**51.**-(1) Kila mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha ataingia katika makubaliano na wateja wake.

(2) Kila makubaliano yaliyoingiwa na mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha wakati wa huduma yake ya huduma ndogo za fedha:

(a) yatakuwa katika maandishi, yanayoweka wazi vigezo na masharti yake yote;

(b) yatamruhusu mkopaji kufanya malipo ya utangulizi ya sehemu au jumla ya kiasi chochote anachodaiwa chini ya mkataba;

(c) yataainisha vigezo na masharti ya malipo ya utangulizi ya kiasi anachodaiwa na mkopaji chini ya mkataba; na

(d) yatakuwa na vigezo na masharti kama itakavyoainishwa.

(3) Kigezo au sharti lolote la makubaliano ambalo linakusudia kumruhusu mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha kwa upande mmoja kubadilisha kiwango cha riba au faida inayolipwa na mkopaji, kipindi cha ulipaji au wajibu mwengine wowote wa mkopaji litakuwa batili.

(4) Endapo mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha atatoa mkopo au kuendeleza mkopo chini ya makubaliano ambayo hayazingatii masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, hakuna riba, faida, tozo au ada nyengine yoyote inayohusiana na mkopo italipwa kwa mkopo mwengine.

(5) Kwa madhumuni ya kifungu hiki neno "makubaliano" maana yake ni mkataba wa mkopo au mkataba wa ukodishaji wa huduma za kifedha.

Ukusanyaji na urejeshaji wa madeni.

**52.**-(1) Deni linalotokana na shughuli za huduma ndogo za fedha chini ya Sheria hii litakusanywa au kurejeshwa kwa namna ilivyoainishwa katika kanuni.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kanuni zilizotungwa chini ya kifungu hiki zitahakikisha kwamba:

(a) hatua za ukusanyaji wa madeni zinachukuliwa kwa utoaji wa taarifa ya maandishi inayojitosheleza kwa mdaiwa;

(b) uchukuaji wa mali ya mdaiwa au usalama wa dhamana kwa madhumuni ya kuuza ili kulipa deni utatumika kama suluhisho la mwisho; na

(c) kipindi kinachofaa kimeainishwa kama taarifa kwa mdaiwa kabla ya kuuza au kuondoa mali iliyochukuliwa ya mdaiwa.

(3) Endapo mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha, bila ya sababu za msingi, atashindwa kufuata masharti ya kifungu hiki, Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa itachukua hatua stahiki ili kuhakikisha masharti yanafuatwa.

## SEHEMU YA NANE
## MASHARTI MENGINEYO

**Adhabu ya jumla**

**53.** Mtu ambaye anakiuka masharti yoyote ya Sheria hii ambapo hakuna adhabu maalumu inayotolewa, ametenda kosa na endapo akitiwa hatiani:

(a) kwa upande wa Daraja la Pili, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Tano za Kitanzania na isiyozidi Shilingi Milioni Ishirini za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi tisa na kisichozidi miaka mitano au vyote viwili faini na kifungo;

(b) kwa upande wa Daraja la Tatu, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Mbili za Kitanzania na isiyozidi Shilingi Milioni Kumi za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita na kisichozidi miaka mitatu au vyote viwili faini na kifungo; na

(c) kwa upande wa Daraja la Nne, atalipa faini isiyopungua Shilingi Laki Tano za Kitanzania na isiyozidi Shilingi Milioni Moja za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi mitatu na kisichozidi mwaka mmoja au vyote viwili faini na kifungo.

**Dhima kwa matendo yanayotendwa na mjumuiko wa watu.**

**54.** Endapo kosa limetendwa chini ya Sheria hii na kikundi cha watu, ama kiwe kimesajiliwa au hakikusajiliwa na kikundi hicho kimebainika kutenda kosa kwa kufahamu au kushiriki au kuhusishwa na tendo au kosa lolote kwa upande wa mtu au watu wowote ambao wanahusika na usimamizi wa kikundi cha watu hao, mtu au watu hao watachukuliwa kuwa wametenda kosa hilo.

Kumaliza makosa.

**55.** -(1) Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa inaweza kumaliza kosa lililofanywa na mtu chini ya Sheria hii au kanuni zake kwa kumtaka kulipa faini isiyopungua nusu ya faini iliyoainishwa kwa kosa hilo, iwapo mtu huyo:

(a) amekubali kwamba ametenda kosa na atachukua tahadhari kwa kutorudia tena kosa; na

(b) atalipa malipo yake yote chini ya Sheria hii.

(2) Taratibu zinazohusiana na kumaliza kosa zitaainishwa katika kanuni.

(3) Kumaliza kosa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, hakutochukuliwa kama ni hatia kwa kosa linaloshukiwa kufanywa na isipokuwa kwamba malipo ambayo hayajalipwa yamelipwa yote, hakutokuwa na mashtaka ya kosa linaloshukiwa yatayofunguliwa au kuendelezwa.

Huduma ndogo za fedha kwa misingi ya kiislamu.

**56.**-(1) Kutakuwa na huduma ya huduma ndogo za fedha inayoendeshwa kwa Misingi ya Kiislamu.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu hiki, watoa huduma wa huduma ndogo za fedha katika uendeshaji wao watafuata masharti ya Sheria hii.

(3) Bidhaa na huduma zote zinazotolewa na watoa huduma ndogo za fedha za Kiislamu zitafuata misingi ya uwezeshaji wa kifedha ya Kiislamu ikijumuisha:

(a) gharama na faida;

(b) mikopo bila ya riba;

(c) mauzo ya awali;

(d) ubia;

(e) kukodisha; na

(f) bidhaa na huduma nyengine zozote zinazoambatana na Shariah.

Jukwaa la Mashauriano.

**57.**-(1) Kutakuwa na Jukwaa litakalojulikana kama Jukwaa la Mashauriano ya Huduma Ndogo za Fedha Zanzibar.

(2) Muundo, kazi na mambo mengine yanayohusiana na Jukwaa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, yatakuwa kama ilivyoainishwa katika kanuni.

Rufaa.

**58.** Mtu yeyote ambaye hajaridhika na uamuzi wa Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa chini ya Sheria hii anaweza, ndani ya siku ishirini na moja kuanzia tarehe ya uamuzi huo, kukata rufaa kwa Waziri kwa mujibu wa taratibu kama ilivyoainishwa katika kanuni.

Taarifa kwa umma.

**59.**-(1) Benki au Mamlaka iliyokasimiwa itachapisha katika Gazeti orodha ya watoa huduma wa huduma ndogo za fedha waliosajiliwa au waliopewa leseni kwa namna ambayo Benki au Mamlaka iliyokasimiwa itaona inafaa.

(2) Wakati wowote usajili wa mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha utakapofutwa au kuondolewa, Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa itatangaza katika Gazeti.

Ushiriki-shwaji wa wazawa.

**60.** Endapo mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha anatoa huduma ndogo za fedha, atazingatia sheria zinazotumika kuhusu ushirikishwaji wa wazawa ikijumuisha ajira na mafunzo kwa Wazanzibari.

Kanuni.

**61.**-(1) Waziri anaweza kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

(2) Bila kuathiri masharti ya ujumla chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Waziri anaweza kutunga kanuni za huduma nyengine za huduma ndogo za fedha ikijumuisha huduma ndogo za fedha kwa misingi ya Kiislamu.

Kufuta na kubakiza.

**62.** -(1) Sheria ya Wakopeshaji Pesa, Sura 166 inafutwa.

(2) Kifungu cha 31 hadi 42 vya Sheria ya Vyama vya Ushirika Zanzibar Nam. 15 ya 2018 vinafutwa.

(3) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) na (2) cha kifungu hiki, kitu chochote kilichofanywa au kuchukuliwa hatua yoyote au kingepaswa kufanywa au kuchukuliwa hatua chini ya masharti yoyote ya Sheria iliyofutwa, kitaendelea kuwa halali na kuchukuliwa kuwa kimefanywa chini ya masharti ya Sheria hii.

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 1 Disemba, 2023.

..............................................

(RAYA ISSA MSELLEM)

***Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.***